

BWANA AMEJAA HURUMA

Zab. 103: 1-4, 6-8, 11

Anga Anselim

Tar. 12, March-2022

Kibosho Senior Seminary

Kwa Uchaji na moyo wa Ibada

Moderato

Soprano
Alto



Bwa na a me ja a hu ru ma na ne e ma,

Tenor
Bass



Bwa na a me ja a hu ru ma na ne e ma.



1. Ee nafsi yangu, umhidi Bwana,
Naam, vyote vilivyo ndani yangu/
Vilihimidi jina lake takatifu*
Ee nafsi yangu, umhimidi Bwana
Wala usizisahau fadhili zake zote.

2. Akusamehe maovu yako yote,
Akuponya magonjwa yako yote*
Aukomboa uhai wako na kaburi,
Akutia taji fadhili na rehema.

3. Bwana ndiye afanyaye mambo ya haki
Na hukumu kwa wote wanaoonewa
Alimjulisha Musa njia zake*
Wana wa Israeli matendo yake.

4. Bwana amejaa huruma na neema
Haoni hasira upesi, ni mwingi wa fadhili*
Maana Mbingu zilivyoinuka juu ya nchi
Kadiri ileile rehema zake ni kuu kwa wamchao.